

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini – Tarehe 8 Juni, 2022**

*(Bunge Lillianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Najma Murtaza Giga) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mkutano wa Saba, Kikao cha Arobaini leo tarehe 8 Juni, 2022. Katibu tuendeleo.

**NDG. YONA KIRUMBI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaanza na maswali Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Seif Said Gulamali, Mbunge wa Manonga, aulize swali lake.

Na. 353

**Serikali Kuunga Mkono Juhudi za Wananchi wa Manonga katika Ujenzi wa Shule**

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuunga mkono wananchi wa Jimbo la Manonga kwa kuwasaidia kujenga madarasa mawili katika kila shule?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa David Ernest Silinde.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inatambua changamoto ya mahitaji ya vyumba vya madarasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2021/2022 Serikali kupitia Mradi wa *SEQUIP* imepeleka shilingi milioni 470 kwa ajili ya ujenzi wa Shule ya Sekondari Seif Gulamali. Pia katika mwaka 2021 kupitia mradi wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO-19 jimbo la manonga lilipokea jumla ya shilingi bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 92 kwa shule za sekondari na shilingi milioni 160 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba nane vya madarasa ya shule za msingi shikizi.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukamilishaji wa vyumba 10 vya madarasa katika Halmashauri ya Wilaya Igaunga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itaendelea kutoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa kadri zitakapopatikana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Seif Gulamali.

**MHE. SEIF K. S. GULAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, kwanza niishukuru Serikali kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa shule za sekondari.

Swali langu la nyongeza, Mheshimiwa Waziri majibu yako yamejumlisha fedha zote zilizopo ndani ya Wilaya ya

Igunga, hivyo basi nilikuwa nataka kuomba kwa shule zetu shikizi kwa maana ya Shule za Kazima, Mwakipanga, Mwamakingi pamoja na Shule ya Msingi Shikizi Mwasung'o. Je, ni lini Serikali itatupatia mkono kutupatia fedha kwa shule hizi shikizi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika Shule ya Sekondari ya Mwisi pamoja na Shule ya Sekondari ya Choma tuna uhaba wa mabwalo la chakula.

Je, ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya mabwalo kwa watoto wanaotumia kidato cha tano na cha sita? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Silinde, Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Seif Khamis Said Gulamali, Mbunge wa Jimbo la Manonga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shule Shikizi ambazo amezianisha Mheshimiwa Mbunge lini tutapeleka fedha, nimuhakikishie tu kwamba zipo katika mipango yetu na bahati nzuri siku ya Jumatatu tumezindua mradi wa *BOOST* na mradi ule unagharimu karibu trilioni 1.1. Kwa hiyo, fedha zile zitakapokuwa zimekuja maana yake tutazipeleka katika shule zote nchini ikiwemo ambazo Mheshimiwa Mbunge ameziainisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile katika mradi huo katika Shule ya Sekondari Mwisi ambazo hazina mabweni ni sehemu ya mpango ambao sisi kama Serikali tutapeleka maana yake ni *component* nzima ni pamoja na mabweni. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Christine Mnzava nilikuona.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa Kata ya Mwasubi iliyopo katika Tarafa ya Mondo, Wilaya ya Kishapu ni kata mpya na haina madarasa ya kutosha katika shule ya sekondari. Je, ni lini Serikali itajenga ili kuongeza madarasa katika shule hiyo? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge tutaongeza madarasa kwa kuwa moja ya mpango wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kuhakikisha shule zote tunazifikia kwa kuongeza madarasa na kuzikarabati. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri tunaendelea na Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Chemba aulize swali lake.

Na. 354

### **Kumalizia Ujenzi wa Maboma ya Zahanati – Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itamaliza ujenzi wa maboma ya zahanati ya Kimu, Rofat, Tumbakose, Songolo na Sori Wilayani Chemba?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Lujuo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2021/2022 imepeleka shilingi milioni 260 kwa ajili ya ukamilishaji wa zahanati 6 za Jangalo, Wairo, Humekwa, Makamaka na Ombiri. Ujenzi wa zahanati hizi umefikia hatua za umaliziaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali imetenga Shilingi milioni 200 kwa ajili ya kukamilisha Zahanati za Nkulari, Nkikima, Mlongia na Handa.

Aidha, ujezi wa maboma ya zahanati ya Rofat, Tumbakose na Songolo ambazo zinajengwa kwa nguvu za wananchi bado hazijafika hatua ya lenta ili kupata fedha ya Serikali kwa ajili ya ukamilishaji.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mohamed Monni swali la nyongeza.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi. Boma la Zahanati la Isusumia limemalizika tangu mwaka 2016. Naomba kujua ni lini sasa Serikali itatenga fedha ili boma lile liweze kumalizika?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, Wilaya ya Chemba kwa ujumla ina maeneo makubwa ya kilimo na hivyo kuna wahamiaji wengi sana. Nini mkakati wa Serikali wa kujenga zahanati kwenye maeneo yale sasa wamehamia watu wengi wa kutosha? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mohamed Lujoo Monni, Mbunge wa Jimbo la Chemba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na boma la Zahanati ya Lusubi ambayo limekamilika tangu mwaka 2016; nitoe maelekezo kwa Wakurugenzi wote wa Halmashauri za Wilaya kote nchini akiwepo Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chemba, majengo yote ya kutolea huduma za afya yakikamilika ni wajibu wao kufuatilia usajili wa zahanati zile, lakini kuweka vifaa tiba vya kuanzia ilia Zahanati zianze kutoa huduma wakati tunasubiri fedha Serikali Kuu kwa ajili ya kuanza kutoa huduma kwenye vituo hivyo kwa maana ya vifaa vya ziada vinavyohitajika.

Kwa hiyo zahanati hii, itafutiwe vifaatiba mapema iwezekanavyo kupitia mapato ya ndani, lakini pia isajiliwe ili ianze kutoa huduma mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na maeneo ya Chemba ambayo yana wananchi wengi, mkakati wa Serikali ni kuhakikisha tunaendelea kujenga zahanati na vituo vya afya kwa maeneo ya kimkakati. Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge aainishe maeneo hayo ya kimkakati Serikali ifanye tathmini na kuona mpango wa utekelezaji. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephat Hasunga nilikuona.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, katika Kata ya Ihanda kuna Kijiji cha Shilanga na Seketu ambazo zina maboma ya zahanati ambayo yamekaa muda mrefu sana. Upi mkakati wa Serikali wa kuhakikisha maboma hayo yanakamilika ili wananchi waweze kupata huduma za afya katika maeneo hayo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Japhet Hasunga, Mbunge wa Jimbo la Vwawa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwapongeze wananchi wa Jimbo la Vwawa kwa kutoa nguvu zao na kujenga maboma ya zahanati, lakini nimuhakikishie kwamba Serikali hii ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kipindi cha mwaka mmoja zaidi ya maboma 900 ya zahanati yaliyoanza ujenzi kwa nguvu za wananchi yamekamilishwa na zoezi hili ni endelevu. Katika mwaka ujao wa fedha tuna maboma 300 ya zahanati kwa ajili ya ukamilishaji. Kwa hiyo tutahakikisha pia katika ukamilishaji huo maboma haya ya Jimbo la Vwawa pia tunayapa fedha kwa ajili ya kuanza kukamilisha kwa awamu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Adamson Mwakasaka nimekuona.

**MHE. EMMANUEL A. MWAKASAKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kama ilivyo Wilayani Chemba, Jimbo la Tabora Mjini lenye Kata 29 wananchi maeneo mbalimbali katika kata hizo wamejenga kwa kujitolea zahanati ambazo sehemu nyingi wamefikia kwenye maboma. Sasa je, ni lini Serikali itasaidia hizo juhudi za wananchi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):**

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Mbunge wa Jimbo la Tabora Mjini kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, maboma haya ya zahanati ambayo yamejengwa na wananchi katika Jimbo la Tabora Mjini ni sehemu ya mkakati wa Serikali kuendelea kuyatambua kwa awamu na kuyatengea fedha kwa ajili ya kuyakamilisha. Ni sehemu ya bajeti ya maboma 300 katika mwaka ujao, tunajua hatuwezi kumaliza yote, lakini tutakwenda kwa awamu katika majimbo yote likiwepo Jimbo hili la Tabora Mjini. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kunti Majala nimekuona.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zahanati ya Mwaiksabe majengo yake yamekuwa ni ya muda mrefu lakini pili walikuwa hawana jengo la mama na mtoto; wananchi wale wamejenga jengo la mama na mtoto na mpaka wamepaua.

Je, Serikali ni lini itawapelekea fedha kwa ajili ya kukamilisha hatua zilizobaki kwa maana ya plasta pamoja na vifaatiba? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze wananchi hawa katika zahanati hii kwa kutoa nguvu zao na kujenga jengo la mama na mtoto na hicho ni kipaumbele cha Serikali. Naomba nitoe maelekezo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri kufanya tathmini ya gharama zinazohitajika kukamilisha jengo hilo ili tuone kama wanaweza kutumia fedha za mapato ya ndani kukamilisha au Serikali Kuu. Lakini nikuhakikishie



kwamba vifaatiba Serikali imetenga bilioni 69.9 mwaka ujao wa fedha tutapeleka pia katika jengo hilo. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Jonas Mbunda.

**MHE. JONAS W. MBUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Changamoto iliyopo katika Wilaya ya Chemba inafafana sawa na changamoto zilipo katika Jimbo la Mbinga Mjini. Kuna zahanati katika vijiji vya Mzopai, Mundeki, Mikolola, Maande na Rudisha nguvu za wananchi zimewekezwa pale.

Kwa hiyo, nilitaka nijue ni lini Serikali itafanya mkakati kuhakikisha kwamba inakamilisha ujenzi wa zahanati ile?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wakati unaendelea kujibu naomba utulivu ndani ya Bunge, sauti zimekuwa za juu, tusikilizane ili tuone majibu ya Waheshimiwa Mawaziri.

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunda, Mbunge wa Jimbo la Mbinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, majengo haya ya maboma ya zahanati katika Jimbo la Mbinga Mjini, kwanza tunawapongeza wananchi kwa kutoa nguvu zao kwa sababu huu ndiyo mpango wa maendeleo ya afya ya msingi kuchangia nguvu za wananchi katika ujenzi wa vituo hivi, lakini nimhakikishie kama ambavyo Serikali imeendelea kukamilisha maboma katika mwaka huu zaidi ya maboma 900 ya zahanati na mwaka ujao 300; tutaendelea pia kutoa kipaumbele katika maboma haya ya Mbinga Mjini ili yaanze kukamilishwa kwa awamu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa George Mwenisongole swali fupi la nyongeza.

**MHE. GEORGE R. MWENISONGOLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Wananchi wa Isansa wamehamasisha kwa kutumia mapato ya ndani ya kituo cha afya wamechanga milioni 56 pamoja na matofali na mchanga; wameanza ujenzi wa wodi ya kinamama na wazazi katika kituo cha afya. Nini kauli ya Serikali katika kuwaunga mkono wananchi hawa Kata ya Isansa?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwenisongole, Mbunge wa Jimbo la Mbozi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa Serikali ni kuendelea kukamilisha majengo ya zahanati na vituo vya afya, hospitali za halmashauri kwa awamu. Kwa hivyo, katika mipango hii tutaendelea pia kuhakikisha tunatambua maeneo haya ya Mbozi ili nayo yaweze kuingia kwenye bajeti kwa awamu kwa ajili ya ukamilishaji wake. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Tunduru Kusini.

Na. 355

**Kuboresha Vituo vya Afya Mchoteka na  
Mtina - Tunduru Kusini**

**MHE. DAIMU I. MPAKATE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Kituo cha Afya Mtina ili kiweze kutoa huduma ya upasuaji pamoja kupeleka vifaatiba katika Kituo cha Afya Mchoteka?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kusini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga shilingi milioni 250 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji, jengo la mama na mtoto na maabara katika Kituo cha Afya cha Mtina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali katika mwaka wa fedha 2022/2023 imetenga shilingi bilioni 47.7 kwa ajili ya ununuzi wa vifaatiba kwa ajili ya vituo vya afya 159 ambavyo vimekamilika ikiwa ni pamoja na Kituo cha Afya Mchoteka, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daimu Mpakate swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri ya Serikali; kwa kuwa Kituo cha Afya Mtina kinahudumia zaidi ya kata nne na changamoto ya kituo kile ni pamoja na kutokuwa na huduma ya upasuaji.

Je, Naibu Waziri anaweza kunihakikishia baada ya Bunge hili atembelee kituo kile ili aweze kuona changamoto za wananchi wa kata ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, kwa kuwa Jimbo la Tunduru Kusini lina kata 15, vituo vya afya vinavyopatikana

mpaka sasa ni vitatu ambavyo vyote havituo huduma ya upasuaji kutokana na tatizo la kutokuwa na vifaa vya upasuaji, lakini kwa kuwa tunahitaji vituo vya afya vingi.

Je, Serikali ina mpango gani ya kuongeza angalau vituo vya afya viwili katika Kata ya Malumba na Kata ya Msechela ambazo zipo mpakani mwa Msumbuji ili kutoa huduma kwa wananchi wale ambao wanahudumiwa kutoka mbali?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali yale Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Daimu Iddi Mpakate, Mbunge wa Jumbo la Tunduru Kusini kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kituo cha Afya cha Mtina, Serikali imeshatenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji. Kwa hiyo, katika mwaka ujao wa fedha tuna uhakika sasa changamoto hiyo tutakuwa tumeondokana nayo, lakini nipo tayari kuambatana na Mheshimiwa Mpakate kwenda kutembelea kituo cha afya hiki na vituo vingine katika Jimbo lake ili kuona utoaji wa huduma lakini pia kuweka mipango ya pamoja kuhakikisha tunaboresha huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na ujenzi wa vituo vya afya katika kata zake 15 tunachukua kata zake mbili na bahati njema Waheshimiwa Wabunge walileta kata tatu za kipaumbele na Serikali inapitia huko kuandaa mpango wa utekelezaji wa ujenzi wa vituo vya afya kwenye kata tatu za kipaumbele kwa kila jimbo. Kwa hiyo, tutafanya hivyo katika jimbo hili la Tunduru Kusini. Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis Ndulane.

**MHE. FRANCIS K. NDULANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Katika Jimbo la Kilwa Kaskazini Serikali ikishirikiana na taasisi ya *Pan African* ilijenga kituo cha afya katika Kata ya Somanga, lakini kituo kile kimekuwa na changamoto kubwa sana ya upatikanaji wa vifaatiba.

Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka vifaatiba ili huduma bora ya afya iweze kutolewa katika Kata ya Somanga?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WA ZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Francis Ndulane, Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan ametenga shilingi bilioni 69.95 mwaka ujao wa fedha kwaajili ya ununuzi wa vifaa tiba kwenye vituo vya afya na hospitali za halmashauri.

Kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa Mbunge wa Kilwa Kaskazini kwamba kituo hiki cha afya ni miongoni mwa vituo ambavyo vitapelekewa vifaa tiba pamoja na vituo vingine vilivyokamilika ili viweze kuanza kutoa huduma za afya. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo ya Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, aulize swali lake.

Na. 356

**Kuanzisha Bodi ya Mitaji kwa Wahitimu wa Elimu ya Juu**

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI** aliuza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuanzisha Bodi ya Mitaji kwa wahitimu wa elimu ya juu kama ilivyo kwa Bodi ya Mikopo ya wanafunzi wa Elimu ya Juu?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, napenda sasa kujibu swali la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianzishwa mwaka 2004 ili kuweka utaratibu wa kisheria unaowawezesha wanafunzi wahitaji wenye sifa ya kujiunga na vyuo vikuu kumudu gharama za elimu ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeupokea ushauri wa Mheshimiwa Mbunge, hata hivyo, Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa vijana kupitia halmashauri kwa kutenga asilimia 10 ya mapato ya ndani. Nashauri wahitimu wa elimu ya juu kutumia fursa hiyo kupata mitaji. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, swali la nyongeza.

**MHE. LATIFA KHAMIS JUWAKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nikushukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri ya Serikali nilikuwa na swali moja la nyongeza.

Je, Serikali inatoa tamko gani sasa kuhakikisha kila muhitimu anapewa kipaumbele anaporudi au anapomaliza au anapohitimu katika elimu yake ya elimu ya juu ili aweze kupata mikopo katika halmashauri waweze kujajiri na ili kuweza kurejesha mikopo kwa wakati? Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Latifa Khamis Juwakali, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye majibu yangu ya msingi kwamba halmashauri zetu zimekuwa zikitenga asilimia 10 ya mapato ya ndani kwa ajili ya kutoa mikopo ambayo ni kwa *ratio* ya 4:4:2 asilimia nne kwa vijana, asilimia nne kwa wanawake na asilimia mbili kwa watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikopo ile inatolewa kwa mujibu wa sheria na zipo kanuni ambazo tumekwenda kuzifanyia marekebisho mwanzoni ilikuwa vijana ni lazima wawe vijana 10 katika kikundi lakini hivi sasa ni vijana tano tu wanaunda kikundi wawe na shughuli maalum ya kufanya na mikopo ile wanaweza kupata.

Kwa hiyo, sisi kauli kama Serikali ni kuwahakikishia tu vijana kwamba wajiunge kwenye vikundi ambavyo ni vya ujasiriamali na sasa hivi haihitajiki kwamba iwe tayari umeshaanza kufanya shughuli hata kama una wazo tu lakufanyakazi fulani au shughuli fulani mikopo ile unaweza kupata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kauli yetu kwa vijana hawa wajiunge kwenye vikundi na kutumia kanuni zile zilizopo kuhakikisha kwamba halmashauri zetu zinawapata mikopo hii ili waweze kukidhi maisha yao, lakini waweze

kurejesha mikopo ile elimu ya juu waliyoichukua. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Rashid Shangazi, Mheshimiwa Ester Bulaya na Mheshimiwa Ritta Kabati.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, majibu ya Serikali yamejikita kwenye mfuko mmoja tu ambao ni asilimia 10 ya mapato ya halmashauri, lakini Serikali inamifuko zaidi ya 45 ya kuondoa umaskini.

Je, haioni sasa ni wakati muafaka wa kuanza kuwakopesha wanafunzi kwa kutumia dhamana ya vyeti vyao ambavyo wamevipata vya kitaaluma ili kuondoa hili tatizo? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Rashid Shangazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Shangazi amezungumza suala la vyeti na mwanafunzi akishapata cheti haitwi tena mwanafunzi anaitwa muhitimu. Kwa hiyo, naomba nilifanyie marekebisho hapo namna gani wahitimu wetu sasa wanaweza kutumia vyeti vyao kuweza ku-access hiyo mikopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba tuchukue ushauri wa Mheshimiwa Shangazi, twende tukaufanyie kazi tuufanyie na tathimini ya kina kwasababu sasa ni suala mtambuka si suala la Wizara ya Elimu peke yake hapa itaingia Wizara Fedha, lakini Wizara ya Vijana na Wizara nyingine ambazo zinashughulika na mambo ya vijana na mikopo kwa ujumla.

Kwa hiyo, naomba tuchukue ushauri wa Mheshimiwa Mbunge twende tukaufanyie tathimini ya kina ili tuweze



kuangalia je, hivi vyeti vinaweza vikatumika kama *bond* ya kuwapatia mikopo vijana wetu. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ester Bulaya.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kuna baadhi ya wizara kama Wizara ya Kilimo mbali ya kwamba kuna mikopo kwenye halmashauri na mifuko mingine wao wamekuwa wakitoa motisha kwa vijana ambao wana *invest* kwenye kilimo. Unapozungumzia tatizo la ajira kwa *graduate* ni kwenye Wizara yako.

Je, hamuoni kwamba kama wizara mnapaswa kuwa na fungu maalum kwa ajili ya kuwasaidia vijana *graduate* wanaoenda kujiajiri wenyewe kama Wizara kama ambavyo mnavyofanya kwenye Bodi ya Mikopo na maeneo mengine? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyojibu kwenye swali la Mheshimiwa Shangazi, sisi Wizara ya Elimu jukumu letu ni kuhakikisha kwamba tunaratibu utaratibu wa utoaji wa elimu nchini. Wanafunzi wakashahitimu linakuwa si jukumu la Wizara ya Elimu, lakini ni jukumu la Serikali.

Kwa hiyo, kwa vile umezungumza habari ya motisha kwa vijana wetu wanaokamilisha masomo yao na kuangalia namna gani tunaweza tukaratibu taratibu zao za kuweza kujiajiri au kupata ajira, tuchukue ushauri huo, lakini Mheshimiwa Ester nadhani baada tu ya kikao hiki kuna umuhimu wa kukaa. Kwa sababu sasa hivi tunafanya mapitio ya mitaala yetu huenda kuna kitu kinakosekana nadhani na wewe unaweza kuwa na *input* na Mungu akipenda tarehe 13 tutakuwa na kongamano kubwa sana pale Dar es Salaam

la kuhakikisha kwamba mitaala yetu ile inakwenda kujibu maswali ya Waheshimiwa Wabunge juu ya suala hili la ajira pamoja na suala la umahiri kwenye masomo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuubebe ushauri wako twende tukaufanyie kazi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo tuweze kuangalia namna gani bora ya kuweza kulifanyia kazi jambo hili. Nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Ritta Kabati nilikutaja.

**MHE. DKT. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niulize swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa sasa hivi kuna malalamiko mengi sana kwa baadhi ya wanafunzi wanufaika wa hii mikopo ya vyo vikiu wamekuwa wakimaliza madeni yao lakini bado mfumo unaendelea kukata madeni yao.

Je, Serikali inasemaje kuhusiana na hawa wanafunzi ambao bado wanaendelea kukatwa wakati wameshamaliza madeni?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kujibu swali dogo la Mheshimiwa Kabati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niweze kumpongeza Mheshimiwa Kabati kwa ufuatiliaji wa karibu wa jambo hili nadhani ameshakuja ofisini si chini ya mara moja/mara mbili kwa ajili ya kufuatilia jambo hili.

Mheshimiwa Kabati kwanza nikuondoe wasiwasi, sasa hivi utaratibu wetu kila mnufaika wa mikopo ile ana akaunti yake na katika akaunti ile inakuwa inaonyesha kwamba kiasi gani amelipa na kiasi gani kilichobaki kwamba hajalipa. Kwa

mantiki hiyo iwapo kama kuna wanufaika ambao wanaendelea kukatwa wakati wameshamaliza ile mikopo, tuna dawati letu la malalamiko la kuonesha kwamba yeye amekamilisha, lakini bado anaendelea kulipwa au anaendelea kukatwa kwenye mishahara au kwenye mafao yake mengine.

Kwa hiyo, hili suala tunaendelea kulifanyia kwa sababu ni suala la kimfumo, lakini nikuondoe wasiwasi wale wote ambao wamekatwa kwa namna moja au nyingine tumekuwa tukizirudisha fedha hizi baada tu ya kuleta hayo malalamiko ili kuweza kuwarudishia wao wenyewe. Nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa majibu ya maswali ya Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto sasa aulize swali lake.

Na. 357

**Kukamilika kwa Kituo cha Polisi cha Wilaya - Lushoto**

**MHE. SHABAN O. SHEKILINDI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Lushoto?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Shabani Omari Shekilindi, Mbunge wa Lushoto kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Lushoto ni kituo cha daraja A kilianza kujengwa mwaka 2014 kwa gharama ya shilingi 417,000,000 na hatua iliyofikiwa ni umaliziaji. Ujenzi wa kituo hicho unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi huu wa Juni 2022. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Shabani Shekilindi.

**MHE. SHABANI O. SHEKILINDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu mazuri na ni kweli kituo kile kinamalizika niishukuru Serikali kwa kutupa fedha milioni 417, lakini pia nimshukuru *IGP* Sirro alikuja kule na akamuomba Mkuu wa Wilaya aitische harambee ya kuchangia majengo ya watumishi, lakini Mkuu wangu wa Wilaya alifanya hivyo na mpaka sasa hivi tunavyosema kuna zaidi ya shilingi milioni 210 kwa ajili ya kujenga nyumba za polisi namshukuru sana Mkuu wangu wa Wilaya na timu yake ya Kamati ya Ulinzi na Usalama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niulize maswali mawili ya nyongeza; Gereza la Lushoto lipo katikati ya Mji wa Lushoto na hivyo kusababisha wafungwa wetu kukosa hata sehemu ya kuota jua, lakini wakati huo huo kuna eneo lipo nje ya mji kidogo wanaita Yogoi.

Je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu wa kwenda kujenga gereza hilo maeneo ya Yogoi na ambako ndiyo kwenye nafasi kubwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; Wilaya ya Lushoto ina wakazi wengi sana kama unavyofahamu, lakini ina taasisi nyingi za binafsi na za Serikali, lakini ikitokea changamoto ya majanga ya moto huwa wanapiga simu Korogwe ambayo kutoka Lushoto kwenda Korongwe ni kilometa zaidi ya 70. Kwa hiyo, mara nyingi wananchi wetu wanapata hasara.

Sasa basi niombe Serikali, je, Serikali haioni kuwa kuna umuhimu au ulazima haraka kujenga kituo cha zimamoto katika Wilaya ya Lushoto? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani Nchi, majibu ya maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Shekilindi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimshukuru kwa kutambua juhudi za Wizara lakini na hususani Jeshi la Polisi kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa kituo cha polisi pale Lushoto. Lakini nimshukuru pia DC kwa harambee aliyofanya kupata shilingi milioni 210 kwa ajili ya nyumba za wafanyakazi, nadhani ni jambo jema la kuigwa na maeneo mengine.

Sasa kuhusu gereza la Lushoto ambalo tunatambua liko katikati ya mji na eneo lile ni finyu ni kweli baada ya Wizara kuona changamoto hizo inayo mpango wa kuhamishia gereza hilo eneo ya Kambi ya Yogoi ambayo iko nje kidogo ya Mji wa Lushoto. Kwa hiyo, pale itakapopata fedha za ujenzi wa gereza hilo, gereza hilo tutalihamisha ili jengo lililopo lifanye kazi nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na lingine kuhusu ombi lake la zimamoto tunalipokea ni suala tu la kibajeti tutakapo kuwa tumepata fedha tutajenga Ofisi ya Zimamoto ndani ya Wilaya ya Lushoto. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Juliana Shonza nimekuona.

**MHE. JULIANA D. SHONZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; kwa kuwa Songwe ni Wilaya naomba kufahamu ni lini sasa Serikali itatujengea Kituo cha Polisi katika Kata ya Mkwajuni chenye hadhi ya Kiwilaya? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge wa Songwe kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyowahi kusema kwenye majibu yetu ya msingi ujenzi wa vituo vya polisi vya wilaya na mikoa utaendelea kadri tutakavyopata fedha, kipaumbele kwa mwaka ujao ni kujenga Makao Makuu ya Mikoa na baada ya hapo tutaingia kwenye wilaya zetu. Kwa hiyo, tutakapopata fedha tutajenga ndani ya Wilaya ya Songwe. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Oran Njeza nilikuona.

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana; kwa kuwa wananchi wa Wilaya ya Mbeya, Jimbo la Mbeya Vijijini wameweza kujenga Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mbalizi na sasa kuna mahitaji makubwa ya kujenga kituo katika Kata ya Igoma na Kata ya Ilembo.

Je, ni lini Serikali itaunga mkono nguvu za wananchi kwa ujenzi wa vituo hivyo viwili? Ahsante

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri Majibu, kwa ufupi ya swali hilo la nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali mawili ya Mheshimiwa Mbunge wa Mbeya Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza tuwapongeze wananchi wa kata hizo mbili ambao wameanza ujenzi wa vituo vya polisi vya kata zao, naomba nikubaliane na Mheshimiwa Mbunge kwamba Wizara itatuma wataalam kutoka Jeshi la Polisi kwa ajili ya kufanya tathimini kuona kiwango cha ujenzi kilichofikiwa, kiasi gani cha fedha kinahitajika ili kumalizia tuweze kuingiza kwenye mpango wetu wa bajeti wa kumalizia vituo ambavyo vimejengwa kwa nguvu za wananchi. Kwa hiyo, tunaomba awe na subira kidogo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma nilikuona na Mheshimiwa Anatropia,

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru..

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asha Juma nimemtaja halafu wewe. *(Kicheko)*

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Kyerwa ni moja kati ya Wilaya mpya...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia nilimtaja Mheshimiwa Asha Juma halafu wewe.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, oh *okay*. *(Kicheko)*

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara kadhaa Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakisimama na kuomba kujengewa vituo au kukarabatiwa.

Sasa ni lini Serikali itaandaa mpango mzima utakoonyesha orodha wa vituo vinanavyotaka kujengwa au kukarabatiwa kwa nchi nzima ili kuwapunguzia waheshimiwa kusimama kuomba vituo mwaka nenda mwaka rudi? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nijibu swali la Mheshimiwa Asha Juma Mshua kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapokea ushauri wako na kwa kweli Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi imeandaa mpango mkakati wa kuboresha sekta ya usalama wa raia ikiwa ni pamoja na uimarishaji wa majengo. Kwa hiyo, ushauri wa kuleta mwongozo hapa unaoonyesha kituo gani

kitajengwa lini au kitakarabatiwa lini tutauandaa tuweze kuuleta kwa Waheshimiwa Wabunge ili kwa kweli kupunguza maswali mengi ya nyongeza ambalo jibu lake linakuwa kama vile linafanana. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Anatropia swali fupi la nyongeza.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Halmashauri ya Kyerwa ni moja kati ya Wilaya mpya ambayo pia haina Kituo cha Polisi, hivyo *OCD* utumie ofisi ndogo ambayo iko Kagenyi, wananchi tayari wameanza tayari ujenzi wa kituo cha polisi cha wilaya.

Nataka nijue ni lini Serikali itawapelekea fedha ili waweze kumalizia ujenzi ambao wameuanzisha kwa nguvu zao wenyewe? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:- *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunatambua uwepo wa halmashauri au wilaya nyingi ambazo hazina vituo vya polisi vya Wilaya kwa maana ya *OCDs officce* na niwashukuru halmashauri ambazo wanatoa majengo kwa ajili ya kutumiwa na wenzetu wa polisi ni muahidi tu Mheshimiwa Mbunge kama ambavyo nimekuwa nikisema katika majibu ya nyongeza hapa, ya maswali ya msingi tunaendelea kujenga vituo vya polisi kwenye mikoa na wilaya ambazo hazina kabisa vituo hivyo. Kwa hiyo, Wilaya ya Kyerwa ni moja ya wilaya ya kipaumbele hasa ukizingatia kwamba iko mpakani pale ambapo itatokea tutapata fedha tutaipa kipaumbele cha juu. Nashukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kakoso nilikuona.



**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi; Wilaya ya Tanganyika ni wilaya ambayo ipo pembezoni mwa mipakani, ni wilaya ambayo haina kabisa kituo cha polisi na wananchi wamejiotolea kupitia hamasa ya Mkuu wa Wilaya wameanza kutoa michango ya kujenga kituo cha polisi.

Je, ni lini Serikali itawapelekea fedha ili wananchi hao waweze kupata kituo cha polisi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokwishajibu kwenye suala la Kyerwa, Wilaya zote za mpakani ni kipaumbele cha Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kuona kwamba zinapata vituo vya polisi kwa ajili ya kuimarisha usalama wa raia na mali zao.

Kwa hiyo, pale ambapo tutapata fedha Wilaya ya Tanganyika itajengewa kituo cha polisi kama ambavyo tumeahidi katika bajeti yetu iliyosomwa na Waziri wangu hapa mwezi mmoja uliopita.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo hiyo na sasa ni swali la Mheshimiwa Asia Abdugarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum.

Na. 358

### **Kumaliza Ujenzi Jengo la Uhamiaji Manyara**

**MHE. ASIA A. HALAMGA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kumaliza ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo la Ofisi ya Uhamiaji Mkoa wa Manyara ulianza mwaka 2012 kwa kutumia Mkandarasi aitwaye *MS Mavonda's Co. Ltd* kwa gharama ya shilingi 862,167,729. Ujenzi huo ulipofikia asilimia 65 zilijitokeza changamoto katika kutekeleza mkataba hali iliyosababisha kuvunjika kwa mkataba huo mwezi Agosti, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imepanga kukamilisha utekelezaji wa mradi huo kwa utaratibu wa nguvu kazi kwa maana ya *Force Account* ambapo taratibu zote zimekamiliika na tayari kiasi cha fedha shilingi 353,986,150 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo zimepokelewa kutoka Hazina. Ujenzi wa jengo hilo unatarajia kukamilika mwezi Oktoba, 2022. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Asia Abdulkarimu Halamga swali la nyongeza.

**MHE. ASIA A. HALAMGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwanza nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa kutengwa kwa kiwango hicho cha fedha na mwezi Oktoba jengo hilo litakuwa limekamiliika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu la nyongeza; kwa kuwa kwa sasa Mkoa wetu wa Manyara tuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa hati za kusafiria lakini pamoja na hati za makazi. Inatulazimu kupata huduma hiyo

Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Dodoma na Mkoa wa Singida na siyo Mkoa wa Manyara.

Je, Serikali iko tayari sasa kutufungia elektroniki ili tuweze kupata huduma hiyo ndani ya Mkoa wetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini swali la pili; kwa kuwa Mkoa wa Manyara uko pembezoni na wahamiaji haramu wengi wanatumia kama njia ya kupita kwenda kwenye nchi zingine.

Je, Serikali haioni haja ya kutuongezea watumishi pamoja na usafiri kwa sababu kwa sasa watumishi wetu wanatumia pikipiki badala ya usafiri wa magari?

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali haya, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Halamga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakiri kwamba katika Mkoa wa Manyara huduma za kutoa *pass* kwa *electronics* zilikuwa hazijafungwa kwenye jengo hili kwa sababu jengo lilikuwa halijakamilika. Hivi sasa watumishi wa ngazi ya Mkoa wako kwenye jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Manyara na mimi nimshukuru Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kuwaweka watumishi hawa kwenye jengo lake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini namuahidi Mheshimiwa Halamga, jengo litakapokamilika mifumo yote ya *electronic* ya utoaji wa *pass* zitatolewa kwenye jengo letu la uhamiaji baada ya Oktoba mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu nyongeza ya watumishi na magari, nakubali kwamba Mkoa wa Manyara unalo gari moja tu aina ya *Forde Ranger* liliko ngazi ya Mkoa, Wilayani kule tunatumia usafiri wa pikipiki, lakini pia kuna uhaba wa watumishi kama alivyokwishaeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama Waheshimiwa Wabunge wanakumbuka wakati wa bajeti tulitamka kwamba wapo watumishi 820 ambao wataajiriwa kama watumishi wapya, wako kwenye mafunzo sasa hivi, wanatarajia kuhitimu mwezi Septemba, 2022. Katika mpango wetu wa ugawaji tutazingatia maeneo yenye upungufu mkubwa zikiwemo Wilaya za Mkoa wa Manyara. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Iddi Kassim nimekuona.

**MHE. IDDI K. IDDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo lililoko Manyara ni sawasawa na Halmashauri ya Msalala, Wilaya ya Kahama. Kwa kuwa Kata ya Isaka kumekuwa na ongezeko la wageni mbalimbali na ukizingatia uwepo wa bandari na uendelezaji wa ujenzi wa bandari mpya, hivyo kuongeza idadi ya watu katika Kata ya Isaka. Sasa Serikali ina mpango gani wa kuanzisha kituo cha uhamiaji?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Iddi, Mbunge wa Msalala kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunatambua uwepo wa muingiliano mkubwa wa wananchi pamoja na wageni kwenye eneo lake hasa kutokana na shughuli kubwa za kiuchumi za uchimbaji wa madini na kwa mtaji huo ni halali Wilaya yake kupata ofisi ya uhamiaji. Na sera ya Wizara ni kuhakikisha kwamba kila ilipo wilaya siyo halmashauri na pale Wilaya ya Kahama ipo ofisi yetu ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba watu wote wanaokwenda Msalala waendeleo kutumia huduma zinazotolewa katika ofisi ya wilaya ambayo iko pale Kahama. Lakini patakapotokea umuhimu wa kupanua zile huduma

kuzipeleka kule, tutashirikiana na Mheshimiwa Mbunge kupata majengo kule ili yaweze kutumika kutoka huduma hiyo. Nashukuru.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani kwa majibu ya Waheshimiwa Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Mlimba sasa aulize swali lake.

Na. 359

**Mgogoro kati ya wananchi na TAWA**

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI** aliliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro kati ya wananchi na TAWA katika Bonde la Mto Kilombero?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godwin Emmanuel Kunambi, Mbunge wa Jimbo la Mlimba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeanza kutekeleza maamuzi yaliyotolewa na Baraza la Mawaziri tangu Oktoba, 2021. Utekelezaji wa maamuzi hayo ulianza katika mkoa yenye migogoro ikiwemo Mkoa wa Morogoro hususan Pori Tengefu la Kilombero. Timu ya Wataalam ya Kitaifa ya Utatuzi wa Migogoro ya Ardhi iko uwandani, inaendelea na zoezi la tathmini kwa kushirikisha mkoa, wilaya na wananchi wa maeneo hayo. Aidha, timu hiyo inafanya tathmini ya makazi na shughuli zenye athari kwenye uhifadhi wa vyanzo vya maji

na rasilimali za wanyamapori ndani ya eneo la Pori Tengefu na Bonde la Mto Kilombero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utatuzi wa migogoro hiyo utaanza baada ya tathmini kukamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Godwin Kunambi.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jamhuri kwa niaba ya Mamlaka ya Uhifadhi kwa maana ya *TAWA* iliwashitaki Wenyeviti wawili wa vitongoji ndani ya Kijiji cha Mkangawalo, kesi ya jinai namba 281 kwa kosa la kufanya shughuli za kilimo kwenye hifadhi, na tarehe 27 Septemba, 2021 Mahakama iliwaacha huru watu hawa na kuagiza warudishiwe ardhi yao na mali zao kwa maana ya trekta walizonyang'anywa.

Je, ni lini Serikali sasa itarejesha mali zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, wananchi wa Jimbo la Mlimba ni wakulima, wafugaji na wavuvi. Mamlaka hii ya Uhifadhi kwa maana ya *TAWA* imekuwa ikiwasumbua mara kwa mara. Je, Waziri ni lini sasa atakuwa tayari kuambatana nami kwenda Jimboni pale Mlimba kwenda kushuhudia kero hizi na kuzitatua? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeze ya Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Jimbo la Mlimba...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, punguzeni sauti kidogo tumsikilize Mheshimiwa Naibu Waziri ni mambo ya muhimu sana kusikiliza. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Godwin Kunambi, Mbunge wa Jimbo la Mlimba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala hili ambalo lilikuwa mahakamani na Mheshimiwa Mbunge ametuthibitishia hapa kwamba watuhumiwa hawa wameshaachiwa huru na mali zao zilishikiriwa na *TAWA*, nitoe tu ufafanuzi katika eneo hili, kwamba mtuhumiwa anapokamatwa ushahidi na vitu vyote vinapelekwa mahakamani. Na pale ambapo inathibitika kwamba mtuhumiwa ameshinda kesi, basi mtuhumiwa anarejeshewa mali zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama mali hizi ziko upande wa *TAWA*, nimuhakikishie tu Mbunge kwamba tutaenda kulishughulikia suala hili ili mali hizi zirejeshwe kwa watuhumiwa. Lakini ninavyofahamu tunapopeleka kesi hizi mahakamani, tunapeleka na vithibitisho vyote na vinakuwa chini ya Mahakama. Kwa hiyo, kama iko kwetu basi nimuhakikishie kwamba vitarejeshwa kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na suala hili la pili kwamba niko tayari kwenda kutoa ufafanuzi. Nimhakikishe tu Mheshimiwa Kunambi kwamba wananchi wa Mlimba watambue kwamba Serikali iko kazini na kama nilivyosema, Timu ya Kitaifa ambayo imeteuliwa na Baraza la Mawaziri iko uwandani, inafanya tathmini bila kufanya taharuki yoyote na inashirikisha mkoa, inashirikisha wilaya na wale wananchi tukimaanisha viongozi walioko kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukishatambua Serikali inapaswa kurejesha kama wale ambao tunatakiwa kuwaondoa hifadhini kwamba watalipwa ama hawastahili kulipwa, wananchi watapewa taarifa na baada ya hapo tutaanza kutatua hii migogoro kwa kushirikishana, hatutaenda kwa nguvu kwa kuwa Mheshimiwa Rais alishasema, hataki kuona taharuki.

Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mbunge kwamba pamoja na kuwa ametaka niende kule, lakini kwa kuwa timu ya tathmini iko uwandani, tuiache ifanye kazi. Tunapoenda sasa kuongea na wananchi tuwe na kitu cha kuwaambia wananchi bila kuweka taharuki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie kwamba tutatutua tatizo hili na tutaambatana naye baada ya tathmini kukamilika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Saashisha nimekuona.

**MHE. SAASHISHA E. MAFUWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana; ili kuepusha migogoro na kutengeneza *sense of ownership* kati ya wananchi wa Jimbo la Hai hususan wanaozunguka Mlima Kilimanjaro na *KINAPA*. Tuliandika barua ya kuomba fedha za *CSR* ili kutekeleza miradi kwenye vijiji vinavyozunguka Mlima Kilimanjaro, na tayari Mheshimiwa Naibu Waziri ulipokea, nilikuletea mwenyewe. Je, ni lini Serikali itatuletea fedha hizi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Saashisha, Mbunge wa Hai kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Wizara kupitia taasisi zake huwa tunatoa *CSR* kwa jamii zinazozunguka hifadhi, na Mlima Kilimanjaro una jamii mbalimbali zinazozunguka hifadhi hiyo. Kwa kuwa hapa katikati tulikuwa tuna changamoto ya UVIKO-19 Wizara yetu ilikumbana na changamoto hiyo, hivyo hatukuweza kupeleka *CSR* kwa wananchi kama ambavyo tulikuwa tumepanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wote wa Hai, kwamba sasa hivi utalii umeanza kuimarika vizuri. Tumeanza kupata wageni wengi, tuna uhakika kabisa kwamba ile *sense of ownership* ya



wananchi wa Hai na maeneo mengine yanayozunguka hifadhi ya Mlima Kilimanjaro wataenda kuiona na watafaidika nayo kupitia *CSR*.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Daniel Sillo nimekuona.

**MHE. DANIEL B. SILLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa fursa niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa migogoro kati ya Hifadhi ya Tarangire na vijiji vya Gijedangu, Hayamango, Vilimavitatu na Salama ni vya muda mrefu.

Je, ni nini mkakati wa Serikali wa kuonesha kwamba migogoro hii inafika mwisho ili wananchi wetu waweze kufanya shughuli zao za kiuchumi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo fupi la nyongeza Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Sillo, Mbunge wa Babati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ambavyo nimeeleza kwenye majibu ya nyongeza kwamba, maeneo yote ambayo yamezungukwa na hifadhi, Serikali itahakikisha wananchi wanafaidika na uhifadhi. Tunatambua kwamba hawa wananchi kwa asilimia kubwa wanatusaidia kusimamia maeneo haya. Sisi tuko huku makao makuu na pamoja na kuwa tuna wataumishi wetu walioko kwenye maeneo ya hifadhi, lakini askari peke yake hawawezi kulinda haya maeneo bila kushikirisha wananchi ambao ndiyo hasa wenye uchungu wa haya maeneo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba *CSR* ni moja ya *priority* ya Wizara ama Serikali kuhakikisha kwamba wananchi wanajisikia kwamba ni sehemu ya hifadhi. Hivyo, tutahakikisha

kwamba wananchi wa jimbo lake wanaona umuhimu wa uhifadhi ili waendeleo kutusaidia kusimamia maeneo haya yanayozunguka hifadhi ya Tarangire. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Wizara hiyo hiyo. Mheshimiwa Jeremiah Mrimi Amsabi, Mbunge wa Serengeti aulize swali lake.

Na. 360

**Mgogoro kati ya Hifadhi ya Serengeti, Pori la Akiba la Ikorongo na Vijiji jirani - Serengeti**

**MHE. JEREMIAH A. MRIMI** aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itaweka alama za mipaka katika Hifadhi ya Serengeti na Pori la Akiba la Ikorongo ili kumaliza migogoro na vijiji jirani?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, Mbunge wa Jimbo la Serengeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya kufanya tathmini ya mpaka wa Hifadhi ya Taifa Serengeti na vijiji imekamilika kwenye vijiji sita ambavyo ni Mbilikili, Gwikongo, Bisarara, Machochwe, Nyamakendo na Mbalibali. Zoezi linalofuata ni kuweka alama za kudumu kwenye mipaka ya Hifadhi ya Taifa Serengeti. Kazi hiyo itafanyika kwa njia shirikishi ili kuhakikisha kwamba kila upande unaridhika na zoezi hilo.

Aidha, katika vijiji vya Robanda na Rwamchanga, Serikali iliweka mpaka wa Pori la Akiba Ikorongo kwa kuwashirikisha kikamilifu wananchi wa vijiji hivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jeremiah Amsabi.

**MHE. JEREMIAH A. MRIMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuja kwa timu ya Mawaziri nane ambayo ilitangaza kuongezwa kwa eneo la mita 500 eneo la Kinga katika vijiji vya Mbilikili, Bisarara, Tamkeri, Mbalibali, Gwikongo, Machochwe, Nyamakendo pamoja na Meringa. Pia katika nyakati tofauti mwaka 2008, 2010, 2013 mipaka ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na vijiji hivyo imekuwa ikibadilishwa.

Sasa je, Waziri wa Maliasili pamoja na Waziri wa Ardhi wako tayari kuja Serengeti wakiambatana nami mapema iwezekanaavyo wakiwa na *GN* ya mwaka 1968 yenye ramani namba 14, 15, 4 ili kutatua tatizo hili kwa sababu ni la muda mrefu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali namba mbili; mwaka 1994 Serikali ilipunguza eneo la *Grumeti Game Reserve* pamoja na *Ikorongo Game Reserve* kutoka kilometa za mraba 3,600 kuwa 993.4 lakini mpaka sasa kumbukumbu za Serikali bado hazijafanya mabadiliko hayo. Kwa hiyo, wananchi wa Makundusi, Pakinyigoti, Rwamchanga, Rwabando wamekuwa wakizuiwa kufanya shughuli zao. Je, ni lini mabadiliko hayo yatafanyika? Ahsante.

**MWENYEKITI:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Jeremiah Amsabi Mrimi, Mbunge wa Serengeti, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la mipaka kama ambavyo timu ya Mawaziri nane ilipita kutoa ufafanuzi, lakini pia ikaacha watumishi ambao walikuwa wanafanya tathmini ya namna ya kuja kutoa ufafanuzi juu ya mipaka

hiyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Serengeti na wananchi wa Serengeti kwamba tathmini sasa hivi imeshakamilika na kinachofuata sasa ni kwenda kuonesha mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi Wizara ya Maliasili na Utalii tukishirikana na wizara ya Ardhi tutaenda kufafanua hii mipaka tukiwa na wananchi wa maeneo hayo na lengo ni kuondoa sasa ile vurugu au taharuki ya kutotambua mipaka kati ya hifadhi na wananchi.

Kwa hiyo, niwahakikishie hawa wananchi kwamba tathmini imeshakamilika tunakuja sasa kufafanua utambuzi wa mipaka ni ipi ya hifadhi ni ipi ya wananchi, hilo linaenda kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na swali lake la pili limehusiana na ufafanuzi wa *GN* baada ya kurekebisha eneo la Hifadhi ya Ikorongo; Serikali itaifanyia kazi eneo hili na tutapeleka waraka kwa wananchi kwa maandishi sasa kuonesha kwamba eneo hili litakuwa ni la hifadhi na lile ambalo limeachwa kwa wananchi ili wawe na uwezo sasa wa kufanya shughuli zao za kila siku, tutaenda kulifanyia kazi na tutatoa taarifa kwa wananchi wa Wilaya ya Serengeti.

**MWENYEKITI:** Nimekuona Mheshimiwa Neema Mgaya na Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. NEEMA W. MGAYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Waziri kumekuwa na mgogoro wa muda mrefu sana kati ya Hifadhi ya Kitulo na Vijiji vya Misilo, Lugoda, Igenge, Nkindo na Makwalanga. Je, lini Serikali itamaliza tatizo hili la mipaka kati ya Hifadhi na vijiji hivi? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza ya Mheshimiwa Neema, Mbuge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niwape pole wananchi wa Makete hususan wanaozunguka eneo hili la Kitulo. Nilishawahi kuzungumza na Mheshimiwa Mbunge na nikatoa ahadi kwamba tungeenda kuutatua huu mgogoro, lakini kutokana na changamoto mbalimbali sikuweza kupata huo muda. Lakini ninamuahidi Mbunge na ananitazama hapa kwamba wananchi wa Makete wakae mkao wa kusubiri, tunaenda na Mheshimiwa Mbunge kutatua mgogoro huu. Na mgogoro huu tunaenda kuumaliza ili wananchi waweze kufanya kazi kwa uhuru na hifadhi tuweze kuisimamia vizuri. Ahsante. (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo, nilikutaja na mwisho Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. DKT. JOHN D PALLANGYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza nalo liko hivi; je ni lini Serikali itatua mgogoro kati ya *Arusha National Park* na wananchi wa Kijiji cha Lukungw'ado ambao unatokana na Serikali haikununua bila kushirikisha Serikali ya Kijiji mashamba Namba 40 na Namba 41 ambayo wananchi walikuwa wanategemea kujikimu nakushukuru sana.

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza na Mheshimiwa Pallangyo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti suala la kutatua migogoro ni wajibu wa Wizara ya yale maeneo ambayo hatujayafikia ni mhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakuja kuyatatua, na ukizingatia maeneo mengi yalikuwa kwenye

vijiji 920, lakini kwa yale maeneo ambayo hayakuvingizwa kwenye vile vijiji 920, na migogoro yao ni mipya tumeshaelekeza wananchi kupitia wawakilishi wao watuletee malalamiko haya ili tupite katika maeneo hayo tuweze kutatua migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, migogoro mingine ni ya kufika sisi kama viongozi, kukaa na wananchi tukaisikiliza. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaambatana katika Jimbo lake ili tuweze kutatua mgogoro huu.

**MWENYEKITI:** Namalizia na Mheshimiwa Ester Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru; migogoro ya ardhi kati ya Hifadhi ya Serengeti Wilaya ya Serengeti na Wilaya ya Tarime, Bunda umekuwa ni wa muda mrefu na ambao mingine inapelekea hata kuzuia wananchi kufanya shughuli zao, mathalani Kata ya Nyatwali iliyopo Wilaya ya Bunda ambayo ina vijiji vitatu, cha Serengeti, Tamahu na Nyatwali yenyewe ina wakazi takribani 10,000 na Serikali imepeleka miradi ya umwagiliaji takribani wa bilioni 1.7 na maji safi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini wakazi hao wamezuiliwa kuendeleza makazi yao takribani miaka 10; tunataka kujua ni kwa nini Serikali isiwaache hao wananchi waendeleze na makazi kwa sababu mmeshindwa kuwalipa fidia ili iweze kuondoka takribani miaka 10 sa hivi?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hili Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kuna maeneo mengo likiwemo eneo la Nyatwali ambalo kiuhalisia lilikuwa ni eneo la wananchi, na nipende tu kuwaambia wananchi

wa Nyatwali kwamba hakuna mgogoro isipokuwa wananchi walioko pale wako kihalali kabisa, wanaishi kihalali na Serikali ilishasajili vijiji na wananchi wapo miaka ya tangu 1974, wapo pale. Hilo niwaondoe wasiwasi, hakuna mgogoro isipokuwa yale maeneo hata wewe ni shahidi umekuwa ukiona malalamiko mengi ya Waheshimiwa Wabunge wananchi wao wanalalamika kwamba kwa asilimia kubwa wanachangamoto ya wanyama wakali hususani tembo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na hili wananchi wa Nyatwali ni mojawapo ya maeneo ambayo yana kilio hiki, tathmini ya Serikali ni kuangalia namna iliyobora ya kuepusha hawa wananchi wasiendelee kuteseka na wanyama wakali. Maeneo ni mengi yamezibwa yamewekwa makazi ya kudumu, wananchi wamejenga kwenye maeneo ambayo ni mapito ya wanyama ukiangalia eneo la Nyatwali ni eneo moja wapo ambalo upande mmoja ni *Serengeti National Park*, upande mwingine ndio Nyatwali ilipo na vijiji vya jirani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiruhusu pale wananchi kuendelea kuishi changamoto ya wanyama wakali tutaendelea kulia kila siku kwa hiyo mimi niwaombe wananchi, maeneo yote ambayo tumeyainisha Serikali imesitisha kuleta huduma mbalimbali, Serikali imeshaanza kufanya tathmini wananchi watalipwa kupisha maeneo hayo. Na hili ni tamko la Serikali kwamba ili kupunguza athari za wanyama wakali ni vyema tukatafuta eneo maalum ya mapito ya wanyama kuliachia ili wananchi waishi kwa amani na wanyama waendeleo kupita katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba suala hili tunalishughulikia kwa uhakika na kwa haraka zaidi ili wananchi waweze kuishi kwa amani na Serikali iendeleo na taratibu za uhifadhi ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii kwa majibu ya maswali hayo ya Wabunge.

Tunaendelea na Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, Mbunge wa Momba sasa aulize swali lake.

Na. 361

**Geti la Tunduma Kuzidiwa Katika Kutoa Huduma**

**MHE. CONDESTER M. SICHWALE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itaongeza geti lingine ndani ya Jimbo la Momba kutokana na geti la Tunduma kuzidiwa katika kutoa huduma?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** alijibu: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Mipango, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Condester Michael Sichwale, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kurahishisha biashara kati ya nchi ya Tanzania na Zambia na kuondoa changamoto ya msongamano wa magari katika Kituo cha Tunduma, Serikali inaendelea kuchambua na kutathmini taratibu zilizopo ili kuona kama kuna uwezekano wa kuongeza Kituo cha Forodha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kuondokana na changamoto ya msongamano wa magari ambapo Januari, 2021 Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) iliingia makubaliano na Mamlaka ya Mapato ya Zambia yanayoelekeza hatua mbalimbali za kuchukua kwa kila nchi. Hatua hizo ni pamoja na:-



i. Kuunganisha mfumo wa *TANCIS* wa *TRA* na mfumo wa *ASCUDA World* wa Zambia ili kuiwezesha Idara ya Forodha Zambia kupata taarifa za shehena ya mzigo husika kabla kuwasili mpakani; na

ii. Serikali ya Zambia kufanya maboresho ya miundombinu ya barabara na eneo la kuegesha magari kupitia ufadhili wa *Trademark East Africa (TMEA)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na makubaliano hayo, Serikali kwa upande wa Tanzania imefanya yafuatayo:-

i. Uanzishwaji wa Kituo cha Pamoja cha Forodha ambacho kimesaidia taasisi zote za Serikali kuwa sehemu moja na kuwasiliana kwa haraka; na

ii. Serikali kupitia ufadhili wa *TMEA* imenunua *scanners* tatu ambazo ni *baggage scanner*, *body scanner* na *cargo scanner*. Aidha, *baggage scanner* na *body scanner* zinafanya kazi na *cargo scanner* inatarajiwa kuanza kufanya kazi mwezi Julai, 2022, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Condester Sichalwe maswali ya nyongeza kama unayo.

**MHE. CONDESTER M. SICHALWE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa nafasi, katika majibu ya msingi ya wizara inaonesha wanazungumzia zaidi biashara kati ya nchi ya Zambia na Tanzania, lakini geti la Tunduma ninaongelea ni biashara kati ya nchi ya Zambia na nchi ambazo ziko *SADC* ambazo ni zaidi ya saba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maswali yangu ya nyongeza kama yafuatavyo; kabla ya maboresho ya bandari zetu lile ilikuwa asilimia 70 ya mizigo inapitia geti lile, kwa hiyo tafsiri yake kama tumeboresha bandari zetu na Kongo wameingia kwenye *East Africa* ina maana kwamba nchi zingine zitapitisha mizigo pale.

## NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Je, Serikali haioni kuna ulazima na uharaka sana kuhakikisha wanaongeza geti lingine ili kuboresha huduma na ufanisi unaotakiwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili; kama ambavyo ziko nchi nyingine ambazo tunapakana nazo, mfano Kenya, kuna magezi ya forodha zaidi ya mawili au matatu, mfano Holili, Namanga, Tarakea na lile geti la Mombasa na Mheshimiwa Waziri alifanya ziara kwenye Jimbo la Momba mwaka jana.

Je, hamuoni sasa kuna haja kabisa ya kuhakikisha nchi ya Zambia ambayo inahudumia nchi zaidi ya saba ya SADC kupata geti lingine ndani ya Jimbo la Momba ili kuhakikisha tunaongeza mapato?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya maswali hayo ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Condester Michael Sicalwe, Mbunge wa Momba kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama yanafanana maswali yake yote mawili kwa hiyo ni suala moja na nimesema katika majibu yangu ya msingi kwamba Serikali inafanya uchambuzi na tathmini kupitia katika sehemu hiyo pamoja na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi tukiona Serikali ipo haja ya kuongeza geti basi Serikali yetu ni sikivu, na iko tayari kufanya hivyo, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu hayo.

Tunaendelea na Wizara ya Kilimo, sasa ni swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge wa Lindi Mjini.

Na. 362

**Kujenga Chuo cha Kilimo Lindi**

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Kilimo katika eneo la Ngongo Mkoani Lindi ambapo tayari hekari 120 zimetengwa kwa ajili hiyo?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdallah, Mbunge Lindi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kutambua umuhimu wa kuimarisha huduma za ugani iliamua kuanzisha Vyuo Vya Mafunzo vya Kilimo vya Serikali tangu miaka ya 1930 ili kuendeleza sekta hii hapa nchini. Mpaka sasa vimeshaanzishwa Vyuo Vya Mafunzo ya Kilimo 14 ambavyo vinatoa mafunzo ya fani mbalimbali za kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada kikiwepo Chuo cha *MATI* Mtwara kwa ajili ya Kanda ya Kusini kwa maana ya Lindi na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sasa Wizara inaendelea na ukarabati wa Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo na kuvipatia vifaa vya kufundishia. Hata hivyo, Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza Mradi wa *HEET* ambapo katika eneo hilo la Ngongo kitajengwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kampasi ya Lindi kitakachotoa programu za kilimo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Hamida Abdallah maswali ya nyongeza.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nishukuru kwa majibu ya Serikali, lakini ningependa kujua katika eneo la Ngongo, sisi Manispaa tulishatoa hekari 120; nini msukumo wa Serikali kuhakikisha kwamba fedha zinapatikana na kuwawezesha Chuo Kikuu cha Dar es salaam kuja kujenga Chuo cha Kilimo *campus* ya Lindi? (*Makofi*)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu ya swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamida Mohamed Abdalaah Mbunge wa Lindi Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nachukuwa fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge amekuwa akilifuatilia sana jambo hili na hii si mara ya kwanza kuliulizia. Sisi kama Wizara ya Kilimo tumefanya mawasiliano na wenzetu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia jambo hili limeshaanza na ndani ya muda mfupi ujao wataendelea na taratibu za kuhakikisha kwamba mchakato huu unakamilika, ili ujenzi uanze mara moja.

Kwa hiyo, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba Serikali inafanya kazi kwa pamoja na wenzetu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia chini ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam wako tayari kuendelea na mchakato huu na hatua zimefikia sehemu nzuri.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Cosato Chumi nilikuona.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Mwenyekiti nashukuru kwa kuniona na kunipa nafasi.

Rais Samia Suluhu Hassan ameonesha nia ya kuimarisha na kuboresha kilimo na kiasi kwamba tumeongeza bajeti yetu ya kilimo; je, Serikali iko tayari kwa kushirikiana na Vyuvo vya Kilimo kutusaidia sisi wananchi huko vijijini kwa kutuletea wale wanafunzi ambao wanakuwa kwenye

mafunzo ya vitendo ili waje kushirikiana na wananchi katika kuimarisha nakuboresha kilimo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cosato Chumi, Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa na programu hiyo ya kuwahusisha wale vijana ambao wako chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia programu ya uhanagenzi na tutaendelea kuifanya hivyo kuhakikisha kwamba wanafikia maeneo mengi zaidi lengo hapa ni kuhakikisha kwamba wanawafikia wakulima wengi zaidi, na wakulima wanapata elimu ya kilimo bora ili kuongeza tija na kufikia malengo ambayo tumejiwekea ya kukuza Sekta ya Kilimo kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Nusrat Hanje atamalizia.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, kwanza naipongeza Serikali katika kuhamasisha kilimo na huduma za ugani suala langu Serikali kupitia Wizara ya Kilimo imenunua pikipiki kwa ajili ya Maafisa Ugani, lakini bado pikipiki hayo hayajagawiwa ili kuepusha uchakavu, ni lini Serikali itayagawa pikipiki hizo kwa walengwa ili yakafanya kazi kwa wakulima? Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri kama zipi hizo mapikipiki ni lini sasa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli bajeti ya Wizara ya Kilimo na hasa katika eneo la huduma za ugani, imeongezeka kutoka shilingi milioni 600 mpaka shilingi bilioni 15 kwa ndani

ya miaka miwili kazi kubwa ambayo Mheshimiwa Rais ameifanya na ndani ya bajeti hiyo pia na sisi tulinunua vifaa kwa maana ya pikipiki, kwa ajili ya kuwapatia Maafisa Ugani. Nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge kwamba zilikuwepo na taratibu za ndani za kuzifuata ambazo zimekamilika na kuanzia jana zoezi la usambazaji pikipiki limeanza, jana Mkoa wa Dodoma wamechukuwa pikipiki 264, leo Singida watachukuwa 161 na kesho kutwa Tabora na maeneo mengine wataendelea kuzichukuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Mheshimiwa Mbunge nikuondoe hofu pikipiki zile ndani ya muda mrefu zitaondoka eneo hilo ili ziweze kuwafikia Maafisa Ugani.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mwongozo wa Spika.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Kunambi hapa

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Nusrat Hanje endelea na swali, Mheshimiwa Kunambi kaa kwanza chini.

**MHE. NUSRAT S. HANJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuwa Kanda ya Kati hususani Mkoa wa Singida na Dodoma ni miongoni mwa mikoa ambayo ni ya kimkakati hususani kwenye zao la alizeti ukiwemo mkoa wa kwako Mheshimiwa Naibu Waziri.

Je, Serikali haioni haja ya kuhakikisha kwamba sasa tunapata Chuo cha Kilimo kwenye Kanda ya Kati kuhakikisha kwamba fedha zinazotengwa na Serikali zinakuwa na tija?

**MWENYEKITI:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo.

**NAIBU WAZIRI KILIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nusrat Hanje, Mbunge wa Viti Maaalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vyetu vya kilimo vimegawanya katika kanda na Kanda ya Kati pia yenyewe inapata huduma kupitia vyuo hivi, lakini sambamba na hizo tunazo taasisi mbalimbali ambazo zinafanya kazi katika Mkoa wetu wa Dodoma pamoja na Singida ambazo lengo lake kuu ni kuhakikisha kwamba tunawajengea uwezo wakulima wetu kulima kilimo cha alizeti kwa tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuondoe hofu Mheshimiwa Mbunge ya kwamba tumezingatia sana ikolojia ya Dodoma na Singida na tumeweka nguvu ya kutosha kuhakikisha wakulima wetu wanapata elimu ya kutosha juu ya kilimo cha alizeti na mwisho wa siku tuondoe tatizo la upungufu wa mafuta ambalo tunalo hapa nchini.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa majibu ya maswali hayo ya Wabunge nakushukuru sana.

**MHE. GODWIN E. KUNAMBI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwongozo wa Spika.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa naomba ukae kwanza.

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru sana kwa kazi nzuri ambayo tumefanya kuanzia asubuhi, lakini niendeleee kuisitiza tu kwanza maswali yetu tujifunze na tuendeleee kujifunza yawe mafupi ya kibunge, lakini pia mawaziri nao wajitahidi kujibu hata yale maswali ya nyongeza kwa ufupi zaidi ili Wabunge wengi wapate fursa ya kuuliza maswali kwa ajili ya maeneo yao. *(Makofi)*

Lakini kabla sijasoma tangazo Waheshimiwa Wabunge sisi Bunge ni taasisi yenye hadhi na heshima pekee katika nchi yetu na hata duniani, na humu ndani kuna wageni wengi wanakuja hususani wanafunzi, kwa hiyo mnapokuwa mnaongea zaidi mpaka sauti zikasikika na mimi nikasema, kule tutakuwa tunawafundisha vibaya wanafunzi wetu. *(Makofi)*

## NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)

Kwa hiyo, naomba tujitahidi tuzungumze kwa sauti za chini ili angalau hadhi yetu iwe nzuri na wanafunzi waige mazuri kutoka Bungeni. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo sasa natangaza wageni ambao wako Bungeni; kwanza ni wageni walioko kwenye Jukwaa la Spika, mgeni wa Bunge ambaye ni Mbunge na Waziri Mstaafu Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe yuko kwenye Jukwaa la Mheshimiwa Spika karibu sana, Mheshimiwa Mgeni wa Bunge. Karibu sana Mheshimiwa Mstaafu Jumanne Maghembe katika Bunge letu. *(Makofi)*

Wageni wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge ambao wapo Bungeni hapa kwa ajili ya kutembelea Bunge letu, naomba wote wasimame kwa umoja wao, Waheshimiwa Wabunge leo hawapo naona. *(Makofi)*

Lakini kuna wageni waliotembea Bunge kwa ajili ya mafunzo kuna wanafunzi 75 na walimu watatu kutoka *High Score Vocational Training Centre* ya Jijini Dodoma, wapo wale pale karibuni sana wanafunzi wetu katika Bunge letu. *(Makofi)*

Lakini pia tuna wanachama 296 na viongozi 30 wa *Red Cross* Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati wakiongozwa na mratibu wao Ndugu Jofrey Mtasiwa wale pale karibuni sana wanachama na viongozi 30 wa *Red Cross* katika Bunge letu. *(Makofi)*

Pia tuna wanafunzi 40 wa Chuo cha *St. John* kutoka Jijini Dodoma wanafunzi wale kule juu karibuni sana wanafunzi wetu. *(Makofi)*

Pia tuna wanachuo 30 na Mkufunzi mmoja kutoka Chuo cha Ustawi wa Jamii Kisangara Mkoani Kilimanjaro, wale pale wapo karibuni sana wanachuo na mkufunzi wao mmoja. *(Makofi)*



*NAKALA MTANDAO (ONLINE HANSARD)*

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijaahirisha shughuli za Bunge nawakumbusha tu baada ya kuahirisha Bunge ile Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi zitakutana ili kuendelea na kazi shughuli za Bunge.

Baada ya kusema hayo naahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 4.20 Asubuhi Bunge lilihahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,  
Tarehe 9 Juni, 2022 Saa Tatu Asubuhi)*